

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati mbili (2) za Kudumu za Bunge zinawaalika wadau kutoa maoni yao kwa njia ya Barua pepe kuhusu Miswada mitatu (3) ya sheria iliyosomwa Bungeni kwa mara ya Kwanza tarehe 7 Februari, 2020, wakati wa Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge. Miswada hiyo na Kamati zilizopelekewa ni kama ifuatavyo; -

- a. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2020 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2020*) – **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.**
- b. Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea wa Mwaka 2020 (*The Plant Health Bill, 2020*)- **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.**
- c. Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa Mwaka 2020 (*The Deep –Sea Fisheries Management and Development Bill, 2020*) - **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.**

Maoni kuhusu Miswada tajwa yawasilishwe kwa Katibu wa Bunge kwa njia ya Barua pepe kupitia anuani zifuatazo:- cna@bunge.go.tz na kamati@bunge.go.tz kabla ya tarehe 04 Mei, 2020.

Miswada husika inaweza kupakuliwa kupitia tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

21 Aprili, 2020.